

Mzigo Flexi FAQ

Mzigo Flexi ni nini?

Mzigo Flexi ni mpango maalum unaokupa fursa ya uwekezaji kwa muda wa miaka mitatu (Miezi 36) huku ukinufaika na faida.

Mzigo Flexi ni kwa ajili ya Mteja wa aina gani?

Mzigo Flexi ni kwa ajili ya wateja binafsi, makampuni au taasisi yoyote yenyewe uwezo wa kuwekeza kwa muda wa miezi 36 kwa riba shawishi. Mfano; Wafanyakazi, Wafanyabiashara, Wakulima, Wafugaji, Vikundi/Vikoba na Wastaafu

Ninahitaji kuwa na vigezo gani ili kupata Mzigo Flexi?

- Umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- Mtu yeyote anaweza kufungua akauti ya CRDB na kuanza uwekezaji huu. Ni rahisi na haina usumbufo

Najiungaje na Mzigo Flexi?

Kujiunga na Mzigo Flexi, tembelea tawi lolote la benki ya CRDB liliyo karibu yako. Pia unaweza kupakua fomu ya maombi mtandaoni.

Je Mzigo Flexi inatoa faida/riba?

Ndio, Mzigo Flexi inatoa faida ya 9% kwa mwaka na malipo ya faida yaweza kulipwa kwa mwezi, robo mwaka, nusu mwaka, mwaka au siku ya kuiva ya amana iliyowekezwa. Mteja anachagua mwenyewe namna ya kupata faida yake.

Je ninaweza kuchagua muda wa kupokea faida?

Ndio, unaweza kupokea faida kila mwezi au kila baada ya miezi 3 au kila baada ya nusu mwaka au kila mwaka au wakati wa ukomo wa uwekezaji.

Nitapokeaje faida inayotokana na Mzigo Flexi?

Faida itawekwa kwenye akaunti yako ya CRDB.

Je ninaweza kuwa na Mzigo Flexi zaidi ya moja?

Ndio, unaweza kuwa na Mzigo Flexi zaidi ya moja na kila uwekezaji utakua unajitegemea

Je kuna kipindi maalum cha kujiunga na Mzigo Flexi?

Ndio, uwekezaji wa Mzigo Flexi utapatikana kwa miezi miwili kuanzi tarehe 17 Mei 2022

Ninaweza kupata Mzigo Flexi kwa fedha za kigeni?

Unaweza kupata Mzigo Flexi kwa Shilingi za Tanzania pekee. Kama una fedha za kigeni utoalamika kuzibadilisha kupata shilingi ili kuwekeza kwenye Mzigo flexi

Je kuna Kiwango cha chini cha uwekezaji kwenye Mzigo Flexi?

Ndio, kiwango cha chini cha uwekezaji ni TZS. Milioni 1. Lakini, unahamasishwa kuweka zaidi ya TZS Milioni 1 ili kupata faida zaidi.

Je ninaweza kupata kadi ya benki nikiwa na Mzigo Flexi?

Wateja wote wanapata kadi ya benki lakini kadi hiyo haitawezza kuona Mzigo flexi. Kadi hiyo itaunganishwa na akauti ya kawaida ya mteja.

Je ninaweza kupata kitabu cha hundi, SimBanking au huduma za kibenki kupitia mitandao?

Wateja wetu wote wanaweza kuomba hundi, Simbanking, intaneti ambazo zinaunganishwa na akauti yake awali. Huduma hizi hazitaunganishwa na Mzigo Flexi kwakua huu ni uwekezaji maalum.

Je kuna makato yoyote kwenye Mzigo Flexi?

Hapana, hakuna makato.

Ninaweza kuendelea na uwekezaji (Mzigo Flexi) baada ya miaka mitatu kuisha?

Ndio, unaweza kuendelea kwa riba ya wakati huo

Ninawekaje Amana kwenye Mzigo Flexi?

- Unatakiwa kuwa na akaunti ya CRDB yenyewe amana ya kuwekeza. Kama hauna akaunti unaweza kufungua akaunti kwa urahisi na haraka bila usumbufo kupitia matawi yetu au Simbanking.
- Kiasi cha kuwekeza kitatolewa kwenye akaunti yako na kuwekwa kwenye Mzigo Flexi.

Ninaweza kusitisha Mzigo Flex kabla ya muda wa ukomo?

Ndio, unaweza kusitisha Mzigo Flex pale utakapoleta Maombi kwenye tawi la CRDB. Hata hivyo utapoteza asilimia hamsini ya faida kama utasitisha uwekezaji kabla ya muda kuisha.

Mzigo Flexi FAQ

Mzigo Flexi ya Milioni 5					
Maelezo	Mwezi	Robo Mwaka	Nusu Mwaka	Mwaka	Ukomo
9% Faida ya mwaka	37,500	112,500	225,000	450,000	1,350,000
10% kodi	3,750	11,250	22,000	45,000	135,000
Kiasi utakachopokea	33,750	101,250	202,500	405,000	1,215,000

Mzigo Flexi ya Milioni 10					
Maelezo	Mwezi	Robo Mwaka	Nusu Mwaka	Mwaka	Ukomo
9% Faida ya mwaka	75,000	225,000	450,000	900,000	2,700,000
10% kodi	7,500	25,000	45,000	90,000	270,000
Kiasi utakachopokea	67,500	202,500	405,000	810,000	2,430,000

Mzigo Flexi ya Milioni 20					
Maelezo	Mwezi	Robo Mwaka	Nusu Mwaka	Mwaka	Ukomo
9% Faida ya mwaka	150,000	450,000	900,000	1,800,000	5,400,000
10% kodi	15,000	45,000	90,000	180,000	540,000
Kiasi utakachopokea	135,000	405,000	810,000	1,620,000	4,860,000

Mzigo Flexi ya Milioni 50					
Maelezo	Mwezi	Robo Mwaka	Nusu Mwaka	Mwaka	Ukomo
9% Faida ya mwaka	375,000	1,125,000	2,250,000	4,500,00	13,500,000
10% kodi	37,500	112,500	225,000	450,000	1,350,000
Kiasi utakachopokea	337,500	1,012,500	2,025,000	4,050,000	12,150,000

Mzigo Flexi ya Milioni 300					
Maelezo	Mwezi	Robo Mwaka	Nusu Mwaka	Mwaka	Ukomo
9% Faida ya mwaka	2,250,000	6,750,000	13,500,000	27,000,000	81,000,000
10% kodi	225,000	675,000	1,350,000	2,700,000	8,100,000
Kiasi utakachopokea	2,025,000	6,075,000	12,150,000	24,300,000	72,900,000

Mzigo Flexi ya Bilioni 1					
Maelezo	Mwezi	Robo Mwaka	Nusu Mwaka	Mwaka	Ukomo
9% Faida ya mwaka	7,500,000	22,500,000	45,000,000	90,000,000	270,000,000
10% kodi	750,000	2,250,000	4,500,000	9,000,000	27,000,000
Kiasi utakachopokea	6,750,000	20,250,000	40,500,000	81,000,000	243,000,000